WIZARA YA NISHATI

# News Bulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 58 | Sep 1 - 21 2024



# UJENZI WA KITUO CHA KUPOZA UMEME TUNDURU UIMEFIKIA ASILIMIA 50 - RAIS SAMIA

WIZARA YA NISHATI

+255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**

Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika
Amanzi Kimonjo

**WAPIGA PICHA**

Steven Nyamiti
Henry Kilasila
Mustafa Shahame
Isaya Mwakajana

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga

© NISHATI 2024

# UJENZI WA KITUO CHA KUPOZA UMEME TUNDURU UIMEFIKIA ASILIMIA 50 - RAIS SAMIA

- Lengo ni kuimarisha upatikanaji wa umeme
- Njia hii ya umeme itaiunganisha Mikoa ya Lindi na Mtwara na gridi ya Taifa
- Vijiji 541 vyafikiwa na huduma ya umeme kati ya Vijiji 551 mkoani Ruvuma
- Asisitiza hakuna mwananchi aliyepisha mradi ambaye hatalipwa fidia



Rsis wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia wananchi wakati akihitimisha ziara yake mkoani Ruvuma, Septemba 28, 2024

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema Serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini ambapo inatekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha kupokea umeme cha Tunduru ambacho utekelezaji wake umefikia asilimia 50.

Rais Samia aliyasema hayo Septemba 28, 2024 wakati akihitimisha ziara yake mkoani Ruvuma iliyokuwa na lengo la kujipima ni kwa kiasi gani Serikali imeweza kutekeleza ahadi ilizo zitoa kwa wananchi.

"Ndugu zangu kukamilika kwa mradi huu pamoja na kuunufaisha Mkoa wa Ruvuma lakini pia utapelekea kuiunganisha Mikoa ya Lindi na Mtwara kuiwezesha kupata umeme wa gridi ya Taifa." Amesema Rais Samia.

Aliongeza kuwa, Serikali inafanya juhudi kubwa katika kusogeza huduma za umeme kwenye kila kijiji ambapo Serikali kupitia REA imefikisha umeme kwenye Vijiji 541 kati ya Vijiji 551 vya Mkoa wa Ruvuma na kuongeza kuwa Serikali inaendelea kusogeza huduma kwenye vitongoji mkoani humo.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi ambao bado hawajalipwa fidia ili kupisha utekelezaji wa miradi ya umeme, kupisha utekelezaji kwani Serikali italipa fidia zao na kuongeza kuwa hakuna mwananchi ambaye hata lipwa fidia.

Pia, alitoa wito kwa viongozi wa Serikali na watumishi wa wananchi kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuokoa maisha ya watanzania pamoja na misitu.




Wananchi wa mkoa wa Ruvuma wakiwasikiliza Viongozi wao, septemba 28, 2024






Baadhi ya viongozi walioambatana na Mhe. Raisi katika ziara yake mkoani Ruvuma

# DKT. BITEKO AAGIZA KIGOMA KUINGIZWA KWENYE GRIDI KABLA YA 2025

- Ataka TANESCO kuongeza kasi utekelezaji miradi ya umeme wa gridi
- Aagiza majenereta ya umeme wa mafuta Kigoma kuzimwa mwishoni mwa 2024
- Azindua ujenzi mradi wa umeme Malagarasi 49.5MW
- Atoa neno kuhusu uchaguzi Serikali za Mitaa



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko ( Kushoto) akiweka Jiwe la Msingi katika mradi wa Kufua Umeme Mto Malagarasi MW 49.5, Mkoani Kigoma. Kulia ni Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Thobias Andengenye.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha linatekeleza kwa kasi miradi ya umeme itakayounganisha Mkoa wa Kigoma katika gridi ya Taifa ifikapo mwishoni mwaka huu Mkoa huo usitumie umeme unaozalishwa kwa kutumia mafuta mazito.

Alitoa agizo hilo tarehe 19 Septemba 2024 mkoani Kigoma wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi mradi wa uzalishaji umeme katika mto Malagarasi (49.5 MW), uwekaji wa jiwe la msingi mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV132 kutoka Igamba hadi Kidahwe na Kituo cha kusambaza umeme msongo wa kV 400/220/132/33 cha Kidahwe.

Alisema kuwa, Serikali imekuwa ikitumia shilingi bilioni 35 kwa mwaka kwa ajili ya kununua mafuta kwa kuendeseha majenereta ya kuzalisha umeme huku makusanyo yakiwa ni shilingi bilioni 16 hivyo imekuwa ni hasara kwa Shirika.

Alisema zoezi hilo la uzimaji wa majenereta pia litafanyika kwa mikoa ambayo haijafikiwa na umeme wa gridi.

Alieleza kuwa, Kigoma inaingia kwenye historia ya kuwa na umeme wa gridi wa uhakika kwa kuwa itapata umeme kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo kutoka Nyakanazi kwa msongo wa kV 400 na kV 220, njia nyingine ni kutoka chanzo cha Malagarasi hadi Kidahwe, kutokea Katavi kwa msongo wa kV 400 na laini ya SGR kutoka Dar es Salaam ya kV 220.

Dkt. Biteko alimshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Kigoma ambapo katika Sekta ya Nishati ametoa zaidi ya shilingi trilioni 1.2 katika mwaka wa fedha 2024/2025

ili kutekeleza miradi ya umeme.

Alieleza kuwa, kwa umeme wa gridi kufika Kigoma Mkoa huo sasa unaondoka kwenye historia ya kuitwa mkoa wa pembezoni na kutambulika kama Mkoa wa maendeleo.
Kuhusu kazi ya usambazaji umeme vijijini amesema Vijiji vyote vitapata umeme kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Katika hatua nyingine Dkt. Biteko ametoa mifuko 500 ya simenti ili kuunga mkono juhudi za wananchi ambao wameanza kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kidahwe huku akiahidi kuwa Serikali itajenga kituo kingine cha afya.

Aidha katika Kijiji cha Igamba ambapo kunatekelezwa mradi wa Malagarasi amesema itajengwa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Barabara ya lami ya kilometa 20 .

Dkt. Biteko pia aliipongeza TANESCO kwa kubadilika katika utendaji kazi kwa kujikita katika kupelekea watu umeme ambapo amewataka wasirudi nyuma na kwamba anaona fahari kuongoza Shirika hilo kwa sasa.

Aidha, kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa aliwaasa wananchi kuchagua viongozi kutokana na uwezo wao wa kuwahudumia na siyo kigezo cha fedha.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mhe. Zainabu Katimba amesema Mkoa wa Kigoma umepokea shilingi trilioni 11.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika kipindi cha uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan ikiwemo sekta ya Nishati ambayo imepata zaidi ya shilingi Trilioni moja.

Alisema uwekezaji wa miradi hiyo ya umeme una tija kwani umeme unahitajika katika maeneo mbalimbali mkoani humo ikiwemo Shule 983, Vituo vya Afya 324 na Hospitali za Halmashauri hasa wodi za watoto wachanga na Watoto njiti ambapo kuna vifaa vya kisasa vyenye mahitaji ya umeme.

Alieleza kuwa, uwekezaji huo unaonyesha kuwa umeme mkoani Kigoma unafika kwa kishindo na kumpongeza Dkt. Biteko na uongozi Wizara ya Nishati kwa kufanya kazi kubwa na za kimkakati na kitalam zinazoendelea kuboresha Sekta ya Nishati.

Aliendelea kuwaasa wananchi kufuatilia ratiba zote za uchaguzi wa serikali za mitaa tarehe 11 hadi 20 mwezi huu kutakapokuwa na zoezi la kujiandikisha katika daftari la mkazi na kuchagua viongozi bora wanaoendana na kasi ya Rais Samia.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, CGF (Mst.) Thobias Andengenye amemshukuru Rais, Dkt. Samia kwa miradi ya maendeleo mkoani Kigoma ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake ya kuufungua Mkoa wa Kigoma na hivyo kuwa kitovu cha uchumi ambapo katika kipindi cha miaka mitatu na nusu cha uongozi wake ametoa shilingi trilioni 11 na bilioni 500 kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ya umeme.

Aliahidi kuwa, Mkoa utasimamia vizuri fedha zinazotolewa ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, alisema leo ni siku ya kipekee kwani kuzinduliwa kwa miradi hiyo kunaifanya Kigoma kuwa na uhakika wa umeme kwa kuwa kwa miaka mingi ulikuwa ni mmoja wa mikoa ya pembezoni huku sifa mojawapo ya mikoa hiyo ikiwa ni kutokuwa na umeme wa uhakika lakini kwa sasa ni sehemu kadhaa tu za mkoa huo hazipo kwenye gridi huku miradi ikiendelea.

Alisema Mkoa wa Kigoma sasa utaungwa kwenye gridi kwa kutumia njia saba tofauti za umeme ikiwemo laini ya kV 400 kutoka Nyakanazi, laini ya kV 400 kutoka Katavi, laini ya SGR ya kV220, laini ya kV 132 kutoka Malagarasi na mitambo ya umeme jua iliyopo mkoani Kigoma ambayo itapelekea Kigoma kuwa kitovu cha umeme nchini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga alisema lengo kuu la Mradi wa Umeme wa Malagarasi ni kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme wa uhakika Magharibi mwa Tanzania ikiwemo Kigoma ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika mikoa ya Magharibi mwa nchi ikiwemo Kigoma. Mradi huu utawezesha ongezeko la umeme katika Gridi ya taifa hivyo kuwezesha biashara ya umeme wa kikanda (Southern and Eastern Africa power pools),. pia zaidi ya wafanyakazi 700 wataajiriwa.

Alisema mradi wa Malagarasi utaimarisha hali ya usambazaji wa umeme katika mkoa wa Kigoma na Wilaya zake hivyo kupunguza gharama za uzalishaji wa umeme ambapo kwa sasa baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Kigoma zinapata huduma ya umeme unaozalishwa

kwa gharama kubwa kwa kutumia jenereta za mafuta ya Dizeli kutoka mitambo ya TANESCO iliyopo Kigoma mjini hali inayopelekea kuliongezea Shirika gharama za uendeshaji.

Alizitaja gharama za jumla katika mradi wa Malagarasi ni Dola za Marekani milioni 144.14 (Sh. Bilioni 398) ambapo Serikali ya Tanzania inagharamia Dola za Marekani milioni 4.14 na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inagharamia Dola za Marekani milioni 140 huku mkandarasi wa Bwawa na kituo cha kuzalisha umeme akiwa ni Dongfang Electric International Corporation kutoka China na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya kV 132 Igamba-Kidahwe (km 54) mkandarasi ni Shyama Power India Limited kutoka nchini India. Mradi pia utasambaza umeme kwenye vijiji 7 na kaya 750 zitaunganishiwa umeme.

Alieleza kuwa, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe una sehemu mbili ambazo ni msongo wa kV 400 na msongo wa kV 220/132/33 ambayo itawezesha Mkoa wa Kigoma kuungwa kwenye gridi ya Taifa kutokea kituo cha Nyakanazi ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 87 huku mkandarasi akiwa ni kampuni ya Sean & Hyusong Consortium kutoka Korea.

Alimshukuru Rais, Dkt. Samia kwa kuipa kipaumbele sekta ya nishati huku mfano hai ni mradi wa umeme wa Julius Nyerere ( JNHPP) ambao unaingiza umeme kwenye gridi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe.Kirumbe Ng'enda alimshukuru Rais Samia kwa fedha za utekelezaji wa miradi na kueleza kuwa, Taifa linakua kwa kasi kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa ikiwemo ya umeme kama JNHPP, Malagarasi, uendelezaji Gesi Asilia na usambazaji umeme.

Mohamed Sauko, Mwakilishi kutoka AfDB alimshukuru Rais kwa kushirikiana na Benki hiyo katika miradi mbalimbali ikiwemo ya Reli, umeme na Barabara.

Aliishauri Serikali baada ya kuwa na umeme wa uhakika ijenge laini itakayoenda Burundi kwa ajili ya biashara ya umeme.

# SERIKALI KUVUTIA WAWEKEZAJI UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI- DKT. BITEKO

- Ashuhudia makabidhiano leseni ya uendelezaji Gesi Asilia Kisima cha Ruvuma
- Azitaka TPDC na ARA Petroleum kutoa kipaumbele kwa wazawa katika ajira
- Kitalu cha Ruvuma kuzalisha Gesi futi ujazo trilioni 1.6



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko ( Kushoto) akiweka Jiwe la Msingi katika mradi wa Kufua Umeme Mto Malagarasi MW 49.5, Mkoani Kigoma. Kulia ni Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Thobias Andengenye.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema Serikali itaendelea kuvutia wawekezaji katika tafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi nchini ili watanzania wanufaike na rasilimali zilizopo.

Dkt. Biteko aliyasema hayo Septemba 10, 2024 wakati wa Hafla ya makabidhiano ya leseni ya uendelezaji eneo la uzinduzi wa Gesi kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na ARA Petroleum katika kisima cha Ruvuma Ntorya mkoani Mtwara.

"Yote haya mnayoyaona ni matunda ya kazi nzuri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan." Amesema Dkt.Biteko

Aliongeza kuwa, jitihada za Serikali zinaenda sambamba na kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ili liweze kushiriki kikamilifu kwenye mnyororo mzima wa thamani wa Mafuta na Gesi.

Aidha, ametoa wito kwa TPDC na kampuni ya ARA Petroleum kutoa kipaumbele kwa wazawa katika utoaji wa ajira ili kuwe na muunganiko kati ya wananchi na ukuaji wa uchumi katika maeneo hayo.

Kuhusu maeneo yenye miradi ya Gesi kama Madimba, Msimbati na Songosongo amewataka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kukamilisha upelekaji wa umeme

kwenye maeneo hayo kufikia mwezi Desemba mwaka huu.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Kirumbe Ng'enda amesema utoaji wa leseni ya uendelezaji kitalu cha gesi cha Ruvuma ni hatua kubwa maendeleo nchini.

"Kitalu hiki kitazalisha futi za ujazo trilioni 1.6, hili ni jambo kubwa sana na la kuipongeza Serikali, tunampongeza Rais Samia ambaye yeye ndie jemedari wa mapambano ya kuleta maendeleo nchini.' Amesema Mhe Ng'enda

Aidha kutokana na uwepo wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere ambao hivi sasa unachangia takribani megawati 705 kwenye gridi ya Taifa, Ng'enda ameiasa Serikali kuwa gesi hiyo sasa itoe mchango mkubwa katika nishati safi ya kupikia na katika uendeshaji wa mitambo na kwenye magari.

Awali Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba alisema kuwa Tanzania ina historia ndefu katika matumizi ya Gesi Asilia kuanzia miaka ya sabini baada ya ugunduzi katika visiwa vya Songosongo.

Aliongeza kuwa,ugunduzi wa Gesi Asilia umefungua mlango endelevu wa uhifadhi wa mazingira na kuimarika kwa usalama wa nishati.

# TUOKOE MAISHA YA WATANZANIA KWA KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA - DKT. BITEKO

- Azindua Kampeni ya Pika Kijanja kuhamisha Nishati Safi ya Kupikia
- Aagiza Wizara ya Nishati kushirikiana na wadau Kampeni ya Nishati Safi
- Awaasa Mama na Baba Lishe kuacha kutumia Nishati isiyo safi
- Apongeza Bongo Fm na TBC kutekeleza Ajenda ya Rais Samia ya Nishati Safi ya Kupikia



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wananchi katika Hafla ya Azimio la Kizimkazi Septemba 8, 2024 jijini Dar es Salaam

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt.Doto Biteko ametoa wito kwa Watanzania kuokoa maisha yao kwa kutumia Nishati Safi ya Kupikia ambayo itawaepusha na madhara yanayotokana na Nishati isiyo safi ikiwemo athari katika mfumo wa upumuaji pamoja na vifo.

Dkt. Biteko aliyasema hayo , Septemba 8, 2024 jijini Dar es Salaam wakati wa Hafla ya Azimio la Kizimkazi iliyolenga kuunga mkono jitihada za Rais, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan katika kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya Kupikia ambayo ilienda sambamba na uzinduzi wa Kampeni ya Pika Kijanja inayoendeshwa na kituo cha redio cha Bongo Fm na Televisheni ya TBC.

Dkt. Biteko alisema kuwa, Rais Samia licha ya kuwa kinara wa Afrika kwenye kampeni ya kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya kupikia, pia amedhamiria kuwaondoa kina Mama na Baba Lishe wa Tanzania katika matumizi ya Nishati isiyo safi na pia kuboresha hali zao kwa kutumia Nishati safi ya Kupiki ambapo ametoa mitungi 2,000 kwa kundi hilo kama njia ya uhamasishaji wa nishati hiyo.

" Nipende kumpongeza sana Mhe Rais kwa kuibeba ajenda hii ya Nishati safi ya Kupikia na kwa maono aliyonayo, nitoe agizo kwa Watendaji wa Wizara ya Nishati kuhakikisha Wizara inashirikisha wadau kwenye kampeni hii ili iweze kufanyika kwa ufanisi na hivyo kumuunga mkono Mhe. Rais." Amesema Dkt. Biteko

Akitoa takwimu za hali ilivyo kwa sasa, Dkt. Biteko amesema watu Bilioni 5.8 duniani ndio wanatumia Nishati Safi huku Bilioni 2.4 wakitumia Nishati isiyo safi ambapo Afrika Pekee ina watu milioni 933 wanaotumia Nishati isiyo safi na hivyo kuwataka wadau kuuganisha nguvu kuunga mkono matumizi ya Nishati iliyo safi.

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alisema Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na Baba na Mama Lishe nchini

na ndio mana kwenye hafla hiyo ya Azimio la Kizimkazi wamealikwa ili kuwahamasisha kuondokana na matumizi ya Nishati chafu na hivyo kuboresha mazingira yao ya ufanyaji kazi kwa kuwapatia Mitungi ya gesi kama Nishati mojawapo iliyo safi.

Alisema, kimsingi muktadha wa Mhe Rais kama Kinara wa Nishati safi ya Kupikia Afrika ni utekelezaji pia wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inayoelekeza Watanzania kupatiwa Nishati Safi ya Kupikia kwa wakati na kwa gharama nafuu na ndio maana mitungi takriban 450,000 iliamuliwa iuzwe bei ya ruzuku ili kuwafikia wananchi.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ambao ndio walioandaa kipindi cha Mhe. Rais cha Azimio la Kizimkazi, Bi Dafrosa Kimbory amesema TBC imeamua kuandaa kipindi hicho kupitia kampeni ya Pika Kijanja ili Rais Dkt. Samia awe mfano wa kuigwa na Watanzania katika kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji na uhamasishaji Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia na kuhakikisha ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania wanatumia Nishati Safi ya Kupikia.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati akiwemo Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati ( Petroli na Gesi), Dkt. James Mataragio, Kamishna wa Umeme na Nishati jadidifu, Mha. Innocent Luoga, Wakurugenzi wa Taasisi chini ya Wizara ya Nishati, wadau wa Nishati ikiwemo Shirika la Madini la Taifa (STAMICO),Oryx na Total Energies ambao kwa pamoja wametoa mitungi 2,000 kwa Mama na Baba Lishe ikiwa ni njia ya uungaji mkono wa Kampeni ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Lengo la Kampeni hii ya Kitaifa ni asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati Safi ya Kupikia ofikapo mwaka 2034




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akitoa mtungi wa gesi kwa moja ya mwananchi katika Hafla ya Azimio la Kizimkazi Septemba 8, 2024 jijini Dar es Salaam

# SERIKALI KUENDELEA KUTEKELEZA MKAKATI WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- **Kapinga asema lengo ni kuwafanya Watanzania zaidi ya asilimia 80 kutumia nishati safi ifikapo 2034.**
- **Kwa mwaka huu wa fedha mitungi laki nne kutolewa.**
- **Atoa rai kwa Watanzania kuendelea kuhamasishana matumizi ya nishati safi ya kupikia.**

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa nishati safi ya kupikia utakaowafanya watanzania zaidi ya asilimia 80 kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo Septemba 19, 2024 katika Kongamano la wanawake na mabinti mkoani Geita lenye lililokuwa na lengo la kutoa elimu ya nishati safi ya kupikia, kujadili mada mbalimbali ikiwemo mwanamke na maendeleo.

"Tunahamasisha matumizi ya nishati safi ya ili kulinda afya za watanzania, kuboresha uchumi na kutunza mazingira ambayo yamekuwa yakiharibiwa kutokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia" Amesisitiza Mhe. Kapinga.

Aliongeza kuwa ili kurahisisha matumizi ya nishati safi ya kupikia Serikali imetoa ruzuku kwenye mitungi ya gesi ambapo kwa mwaka jana ilitoa mitungi laki moja na elfu nne na mwaka huu wa fedha Serikali inategemea kutoa mitungi laki nne.

Aidha, Serikali kuendelea kuhakikisha Taasisi zenye watu zaidi ya 100 zinaendelea kubadilishana mfumo na kutumia gesi.




Naibu Waziri Nishati Mhe. Judith Kapinga akizungumza katika Kongamano la Mabinti na Wanawake Kuhusu Umuhimu wa Nishati Safi ya Kupikia Mkoani Geita.

Mhe. Kapinga alisema kuwa, nishati safi za kupikia zipo za aina nyingi ikiwemo gesi, majiko banifu, umeme, majiko ya ethanol na majiko mengine yaliyoboreshwa na kuwa ya nishati safi.

Ametoa rai kwa Watanzania kubadilisha fikra kuwa mapishi ya nishati safi ni gharama na kusisitiza kuwa majiko ya siku hizi yameboreshwa hayatumii umeme mwingi.

Aidha, Serikali inaendelea majadiliano na wadau ili wananchi waweze kununua gesi kidogo kidogo ili kumwezesha mtanzania kununua gesi kulingana na kiasi cha fedha alichonacho.

"Kila mmoja analojukumu la kulinda mazingira kwa ajili ya mama Tanzania, nitoe rahi tuendelee kuhamasishana juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ", Alisema Mhe. Kapinga.



Mbunge wa Geita Mjini Ndg. Constantine Kanyasu akizungumza na Mabinti katika Kongamano la Umuhimu wa Nishati Safi ya Kupikia Mkoani Geita.



Naibu Waziri Wa Nishati Mhe. Judith Kapinga Akiwasili Ukumbi Kwenye Kongamano la Wanawake na Mabinti kuhusu Matumizi ya Nishati Safi Ya Kupikia Mkoani Geita.



Wanawake na Mabinti wakifurahia Jambo Wakati wa Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia Mkoani Geita

# MRAMBA AZIKARIBISHA KAMPUNI ZA UINGEREZA KUWEKEZA KWENYE NISHATI JADIDIFU

- Asema Serikali imeamua Gridi iwe na umeme mwingi unaotokana na Nishati Jadidifu
- Asisitiza Tanzania kuendana na mipango ya Dunia ya uzalishaji umeme kwa kutumia nishati safi
- Uingereza yaipa Tanzania Kipaumbele katika uwekezaji



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (Kushoto) akizungumza na Ujumbe kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania, ukiongozwa na Kiongozi wa Timu ya Ustawi Endelevu Bw. Euan Davidson (wa kwanza Kulia) kuhusu maeneo ya ushirikiano katika Sekta ya Nishati tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Dodoma

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amezikaribisha Kampuni kutoka nchini Uingereza kuwekeza kwenye Sekta ya Nishati hasa eneo la Nishati Jadidifu ili kutimiza lengo la Serikali la kuingiza umeme mwingi kwenye gridi ya Taifa unaotokana na Nishati Jadidifu.

Aliyasema hayo jijini Dodoma wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Ujumbe kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania ukiongozwa na Bw. Euan Davidson, Kiongozi wa Timu ya Ustawi Endelevu ambapo kikao hicho kililenga kujadili maeneo ya ushirikiano.

Mhandisi Mramba ameueleza ujumbe huo kuhusu mahitaji ya uwekezaji kwenye miradi ya nishati jadidifu ikiwemo umeme jua kwa ajili ya matumizi ya majumbani hasa kwenye sehemu zilizo nje ya gridi pamoja na uwekezaji mkubwa wa umeme Jua utakaoingia katika gridi ya Taifa.

Amesema kuwa, tayari uwekezaji kwenye nishati ya umeme jua umeanza kupitia mradi wa Kishapu-Shinyanga (150MW) na uwekezaji mwingine utafanyika kwenye maeneo mengine nchini ikiwemo Mkoa wa Dodoma (200 MW).

Kuhusu uwekezaji katika umeme unaotokana na upepo amesema kuwa, kuna maeneo tayari yameshatambuliwa ambayo yanaweza kuzalisha umeme huo ikiwemo Dodoma, Singida,

Mbeya, Makambako, Same, Mara na Arusha anbayo yanahitaji ushirikiano katika uwekezaji. “ Tanzania tumebarikiwa vyanzo vingi vya Nishati Jadidifu kwani pia tuna hazina kubwa ya Jotoardhi katika maeneo takriban 52 ambayo yakiendelezwa yatazalisha umeme kuliko nchi ya Kenya ambayo sasa inazalisha umeme wa Jotoardhi takriban megawati 1000.” Ameeleza Mramba

Aidha, alieleza nia ya Tanzania kutumia nishati safi zaidi kuzalisha umeme ikiwemo nishati ya blue hydrogen inayotokana na rasilimali ya Gesi Asilia, bila kusahau matumizi ya nishati ya bayogesi hasa katika maeneo ya vijijini yenye mifugo mingi.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, Mhandisi Mramba ameueleza ujumbe huo juhudi zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha asilimia 80 ya wananchi wanatumia iliyo safi kupikia ifikapo mwaka 2034, ameeleza kuwa hii yote ni utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, ambao utekelezaji wake unashirikisha Serikali na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta binafsi.

Kuhusu usambazaji umeme mijini na vijijini, Mhandisi Mramba amesema Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye eneo hilo na kwa usambazaji umeme vijijini asilimia 99 ya vijiji vimefikiwa na umeme na kwamba ifikapo mwezi Disemba mwaka huu kila Kijiji kitakuwa kimefikiwa na huduma ya umeme.

Kwa upande wake, Bw. Euan Davidson, Kiongozi wa Timu ya Ustawi Endelevu kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini, ameshukuru kwa kupata taarifa za kina kutoka Wizara ya Nishati ambazo zitatumika na nchi hiyo kuangalia maeneo wanayoweza kushirikiana na Tanzania katika uwekezaji kwenye Sekta ya Nishati.

Alieleza kuwa mazungumzo ya viongozi hao yamekuwa na umuhimu kwani Tanzania ni moja ya nchi zinazopewa kipaumbele na Uingereza katika masuala mbalimbali ikiwemo uwekezaji.

Mazungumzo ya viongozi hao pia yamegusia Kongamano la Kimataifa la Nishati litakalofanyika Tanzania mwaka 2025 ambapo Uingereza imeonesha nia ya kushiriki.

# WIZARA YA NISHATI ENDELEENI KUUSIMAMIA MRADI WA JNHPP IPASAVYO-KAMATI YA BUNGE

- Mradi wafikia asilimia 98
- Mkandarasi alipwa Sh.Trilioni 6.3 kati ya Sh.Trillioni 6.5
- Kapinga aahidi kuendeleza usimamizi makini



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeitaka Wizara ya Nishati kuendelea kuusimamia ipasavyo Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Julius Nyerere (JNHPP) ili ukamilike kwa wakati.

Hayo yameelezwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Kirumbe Ng'enda Septemba 07, 2024 wakati wa ziara ya kukagua hatua za utekelezaji wa mradi huo ambao utaingiza megawati 2,115 mara baada ya kukamilika.

"Wizara iendelee kusimamia kwa umakini mradi huu ili mashine zote Tisa ziweze kukamilika kama ilivyopangwa." Amesema Mhe. Ng'enda

Aidha, kamati hiyo imeipongeza Serikali kwa kuhakikisha mashine zilizosalia zinaendelea kukamilika na kufanya kazi ambapo hadi sasa zimekamilika mashine tatu ambazo zinazalisha kiasi cha megawati 705 na mashine namba sita ipo kwenye hatua za mwisho kukamilishwa.

Kwa upande wake Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga alisema Wizara ya Nishati imekuwa ikifanya kazi kwa ushirikiano na kamati hiyo ya Bunge ikiwa ni pamoja na kupokea maelekezo, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

"Kazi kubwa ya Kamati ni kutusimamia sisi Serikali, na sisi tunahakikisha kuwa maelekezo yenu yote yanatekelezwa na mafanikio yake yanaonekana katika miradi mbalimbali kama JNHPP ambao utekelezaji

wa mradi wake umefikia asilimia 98." Amesema Kapinga

Aliongeza kuwa, Wizara ya Nishati chini ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko itaendelea kuusimamia mradi huo ila ukamilike kwa wakati.

Alieleza kuwa, Mkandarasi wa mradi ameshalipwa takriba shilingi trilioni 6.3 kati ya shilingi trillioni 6.5 zinazopaswa kulipwa.












# MBINGA WAMSHUKURU RAIS SAMIA UTEKELEZAJI MIRADI YA MAENDELEO

- Ni Umeme, Maji, Barabara, Elimu na Afya
- Mbinga kupata kituo cha umeme cha sh. Bilioni 3
- Shilingi Bilioni 83 yapeleka umeme Vijijini Jimbo la Nyasa



Mheshimiwa Rais Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Wananchi Wa Mbinga wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa Jengo la Halmashauri la Wilaya ya Mbinga Leo Septemba 25, 2024.

Wananchi wa Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma kupitia kwa Naibu Waziri Nishati na Mbunge wa Viti Maalum Vijana Taifa, Mhe. Judith Kapinga wamemshukuru Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ya Umeme, Maji, Barabara, Shule za Sekondari na Msingi pamoja na Afya.

Pongezi hizo zimetolewa Septemba 25, 2024 wakati Mhe. Rais Samia akizindua jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Katika Sekta ya Nishati, Mfano wa miradi hiyo ni ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Mbinga chenye thamani ya shilingi bilioni 3 ambao utatekelezwa katika mradi wa kuboresha gridi ya Taifa Awamu ya Pili.

Aidha kwa upande wa umeme vijijini, katika Jimbo la Nyasa umeme umefika katika Vijiji vyote 84 kwa gharama ya shilingi Bilioni 83.



Naibu Waziri Wa Nishati na Mbunge wa Viti Maalumu Vijana Taifa Mhe. Judith Kapinga akizungumza wakati wa Halfa ya Uzinduzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Septemba 25, 2024.





Naibu Waziri Wa Nishati na Mbunge wa Viti Maalumu Vijana Taifa Mhe. Judith Kapinga akifurahi Pamoja na Madiwani wa Wilayani Mbinga wakati wa Hafla ya Uzinduzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Septemba 25, 2024.



Wananchi wakifatilia Mkutano wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Wakati wa Hafla Ya Uzinduzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Septemba 25, 2024.

# MKAKATI WA MATUMIZI YA MAJI KWA KUZINGATIA MAHITAJI YA KILA SEKTA UMELETA MAFANIKIO- KAPINGA

- Ampongeza Dkt.Biteko kutoa muongozo matumizi endelevu ya maji
- Asema JNHPP ni kielelezo cha matumizi bora ya maji
- Asisitiza Taasisi za Serikali kuendelea kusimamia matumizi bora maji

Imeelezwa kuwa, Mkakati wa ushirikiano uliowekwa na Wizara zinazohusika na Sekta ya Maji ili kutoa elimu ya kulinda vyanzo vya maji pamoja na kushirikiana na jamii kulinda vyanzo hivyo umeonesha mafanikio.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga ameyasema hayo Septemba 24, 2024 mkoani Ruvuma wakati Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alipozindua mradi wa maji katika eneo la Mtyangimbole ikiwa ni muendelezo wa ziara yake mkoani humo.

Kapinga amesema ushirikiano wa Wizara hizo hauishii katika kutoa elimu na kuvilinda vyanzo vya maji pekee bali wanahakikisha maji yanatumika kwa kufuata mahitaji ya kila sekta.

Alisisitiza kuwa kwa kutambua sekta ya maji ni mtambuka, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko aliitisha kikao cha Wizara zote zinazonufaika na Sekta ya Maji kwa nia ya kuweka mikakati ya ushirikiano katika matumizi endelevu ya maji.

"Mfano Wizara ya Maji, Kilimo na Nishati zinategemeana kuhakikisha huduma zetu za umeme zinaenda vizuri, huduma za kuwapatia wananchi maji zinaenda vizuri na huduma nyinginezo kama za umwagiliaji pia zinaenda vizuri kwa kutumia vyanzo ambavyo tunavyo.' Amesema Mhe. Kapinga

Alisema, matunda ya matumizi bora ya maji ni pamoja na mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao sasa mashine tatu tayari zinazalisha umeme kwa kutumia maji ambapo kabla ya kuanza kwa mradi huo uzalishaji umeme kwa kiwango kikubwa ulitemegea chanzo cha Gesi Asilia.

Kuhusu shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo kuharibu vyanzo vya maji, Kapinga alisema Taasisi zote za Serikali zinashirikiana kuhakikisha mazingira yanatunzwa pamoja na kutoa elimu ili kuhakikisha maji hayachepushwi pasipo utaratibu



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga akizungumza na Menejimenti ya Tpdc (Hawapo Pichani) wakati akifungua Kikao Kazi cha Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini ( TPDC) kilichofanyika Jijini Mwanza.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga Akiwa katika Picha ya Pamoja na Mkurugenzi Mtendaji Wa TPDC Ndg. Mussa Makame (Kulia) pamoja na Kamishna wa Petroli na Gesi Mha. Goodluck Shirika (Kushoto) wakati akifungua Kikao kazi cha Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini (TPDC) Jijini Mwanza.



Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC Ndg. Mussa Makame akizungumza na Menejimenti ya TPDC pamoja na Washiriki Wengine Wakati wa Kikao cha Kikao kazi cha TPDC Jijini Mwanza.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga Akiwa katika Picha ya Pamoja na Mkurugenzi Mtendaji Wa TPDC Ndg. Mussa Makame ( Kushoto) pamoja na Kamishna wa Petroli na Gesi Mha. Goodluck Shirika (Kulia) wakati akifungua Kikao kazi cha Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini ( TPDC) Jijini Mwanza.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga Akiwa katika Picha ya Pamoja na Mkurugenzi Mtendaji Wa TPDC Ndg. Mussa Makame ( Kushoto) pamoja na Kamishna wa Petroli na Gesi Mha. Goodluck Shirika (Kulia) wakati akifungua Kikao kazi cha Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini ( TPDC) Jijini Mwanza.

# MASHIRIKIANO PURA, ZPRA YAZIDI KUIMARIKA

Mashirikiano kati ya Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) ya Tanzania Bara na Mamlaka ya Uthibiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar (ZPRA) ya Zanzibar yameendelea kuimarika kufuatia jitihada za dhati zinazofanywa na uongozi wa Taasisi hizo kutekeleza Hati ya Makubaliano waliyoingia mwaka 2022.

Hayo yamedhihirika wakati wa kikao cha menejimenti za PURA na ZPRA kilichofanyika Septemba 24, 2024 Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujadili taarifa ya utekelezaji wa mashirikiano baina ya Taasisi hizo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Kikao hicho kiliongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mha. Charles Sangweni na kuhudhuriwa na Mkurugenzi Mtendaji wa ZPRA, Mha. Mohammed Slum Said, wajumbe wa menejimenti wa Taasisi hizo na wajumbe wa Kamati ya Pamoja ya Ufundi (Joint Technical Committee - JTC) iliyoundwa kuwezesha utekelezaji wa Hati ya Mashirikiano.

Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa Hati ya Mashirikiano iliyowasilishwa na JTC, kwa mwaka 2023/24 PURA na ZPRA zilishirikiana katika maeneo mbalimbali yakiwemo durusu ya mikataba kifani ya uzalishaji na ugawanaji wa mapato, maandalizi ya miongozo ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR Guidelines), mafunzo ya kaguzi za mikataba ya uzalishaji na ugawanaji wa mapato (PSA audits) na uhifadhi wa data za petroli.

Maeneo mengine ni maandalizi ya mkakati wa kunadi vitalu, uzinduzi wa duru ya kwanza ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa upande wa Tanzania Zanzibar na utangazaji wa vitalu hivyo kupitia mikutano mbalimbali ya kimataifa.



Menejimenti za PURA na ZPRA katika kikao kilichofanyika Septemba 24, 2024 Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujadili taarifa ya utekelezaji wa mashirikiano baina ya Taasisi hizo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

# PURA, M&P ZAJADILI MRADI WA UCHORONGAJI VISIMA MNAZI BAY

Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) imefanya mazungumzo na mwendeshaji wa Kitalu cha Mnazi Bay (Kampuni ya Maurel et Prom Exploration Production Tanzania Ltd) kujadili mradi wa uchorongaji wa visima vitatu vya gesi asilia kutoa idhini ya matumizi ya fedha kwa ajili ya mradi huo. Mradi unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani Milioni 80.2

Kati ya visima vitakavyochimbwa, visima viwili (MB5 na MS2) vitakuwa visima vya uzalishaji (infill) wakati kisima kimoja (Kasa) kitakuwa kisima cha ilieleza kuwa inafuatilia kwa karibu kila hatua ya utekelezaji wa mradi huo kuhakikisha watanzania na watoa huduma wa kitanzania wanashiriki kikamilifu.

Kitalu cha Mnazi Bay kina visima vitano vinavyozalisha gesi asilia kwa wastani wa futi za ujazo milioni 74.24 kwa siku (kwa mwezi



Wajumbe walioshiriki kakao kati ya PURA na M&P kilichofanyika Septemba 30, 2024 kwa lengo la kujadili mradi wa uchorongaji wa visima vitatu katika Kitalu cha Mnazi Bay(TPDC) Jijini Mwanza.

unaotarajiwa kutekelezwa mwanzoni mwa mwaka 2025.

Mazungumzo hayo yalifanyika Septemba 30, 2024 katika Ofisi za PURA Dar es Salaam chini ya uenyekiti wa PURA.

Miongoni mwa wajumbe walioshiriki kikao hicho ni pamoja na Bw. Simon Nkenyeli ambaye ni Meneja wa Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia kutoka PURA na Meneja Mkuu wa M&P Bw. Sylvain Pichelin.

Katika kikao hicho, M&P ilitoa ufafanuzi wa bajeti ya mradi, hatua muhimu kabla ya PURA utafutaji.

Kuelekea utekelezaji wa mradi, tathmini ya athari kwa mazingira imekamilika na zoezi la fidia kwa wananchi watakaopisha mradi linatarajiwa kuanza mapema mara baada ya uhakiki kukamilika.

PURA na M&P zilijadilia pia ushiriki wa watanzania na watoa huduma wa kitanzania katika zabuni zinazotokana na mradi huo.

Katika eneo hili, PURA iliitaka M&P kuhakikisha inazingatia matakwa ya Sheria kuhusu ushiriki wa watanzania. Aidha, PURA Septemba).

Wabia katika Kitalu hicho kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ni M&P (ambaye ni mwendeshaji) mwenye ushiriki wa asilimia 60 katika shughuli za uzalishaji na TPDC mwenye asilimia 40.

Uchorongaji wa visima vitatu vipya utawezesha kuimarisha uzalishaji (maintenance of production plateau) na kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kijiolojia kuhusu mashapo yaliyo katika Kitalu hicho.